

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE

23 MEI, 2019



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE – TAREHE 23 MEI, 2019

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri linalomhusu Mheshimiwa Stephen Julius Masele (Mb).

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **281. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Shamba la uzalishaji wa Mitamba Kibaha lipo katikati ya Mji wa Kibaha na limezungukwa na makazi ya Watu:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya matumizi ya eneo hili kwa ufanisi zaidi.

## **WIZARA YA MAJI:**

**282. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE:**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mwezi Novemba, 2018 Waziri wa Maji alifanya ziara Wilayani Kakonko na Kibondo na kukagua miradi ya maji iliyokwisha tumia zaidi ya shilingi bilioni moja lakini haifanyi kazi:-

Je, ni lini miradi hiyo itakamilika.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**283. MHESHIMIWA MUSSA BAKARI MBAROUK (TANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Katika Vijiji vya Kigombe Wilayani Muheza na Kipumbwi Wilayani Pangani kuna Bandari buba zinazotumika kwa uvuvi na kusafirisha abiria na bidhaa:-

Je, ni lini Serikali itarasimisha Bandari hizo kwa kujenga Gati pamoja na Kituo cha Forodha.

**284. MHESHIMIWA SUSAN PETER MASSELE  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kutokana na umuhimu wa kimkakati katika nyanja mbalimbali za maendeleo kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na nchi yetu kwa ujumla:-

Je, ni lini Jiji la Mwanza litakuwa na Uwanja wa Ndege unaoendana na hadhi na ukuaji wa kasi wa Jiji hilo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**285. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE  
KABOYOKA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wako tayari kuanzisha Misitu ya Vijiji kwenye maeneo yenye ukame kama vile Kata za Bendera, Kihurio, Ndungu na Maore ili kuhifadhi mazingira.

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha miradi ya utunzaji wa mazingira katika Kata tajwa kwa kufundisha Wanavijiji uanzishwaji wa Misitu ya Vijiji.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **286. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wakati Jeshi la Polisi likitekeleza majukumu yake kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa Haki za Binadamu na hata uvunjifu wa Katiba kwa kisingizio cha maagizo kutoka juu:-

- (a) Je, ni mamlaka gani ya juu iko juu ya Sheria;
- (b) Je, maagizo hayo yanapopingwa na Sheria za nchi na kukiuka Haki za Binadamu nini hukumu ya yule aliyetendewa kinyume cha Sheria;
- (c) Je, huyu anayekutwa na kadhaa hii hana haki ya kumjua huyo mwenye mamlaka ya juu.

## **V. HOJA ZA KAMATI:**

### **MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri linalomhusu Mheshimiwa Stephen Julius Masele (Mb).

## **VI. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:-**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA  
23 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**



**BUNGE LA TANZANIA**